# Jinsi ongezeko la kodi linavyoathiri kilimo cha maua, mbogamboga nchini Tanzania




Mjasiriamali kama huyu anapaswa kujengewa mazingira mazuri ya kibiashara ili akuwe na kufikia hadhi ya mfanyabiashara mkubwa ili aongeze pato la taifa kupitia kodi na kuzalisha ajira. **Picha ya Maktaba.**

**MTAZAMO WA WASOMAJI**

**Elly Kombe**

**Ili kuboresha mazingira biashara ni muhimu mfumo wa elimu ubadilike ili wahitimu waandaliwe kujiajiri na kuwa wajasiriamali badala ya kuwa watafutaji ajira.**

**Serikali iongeze ujenzi wa miundombinu ya kijamii na kiuchumi. Serikali ipunguze urasimu kwenye huduma kama utoaji leseni, vibali na kodi.**

**Musa Semuyemba**

**Kwanza tujihoji na viongozi wetu wajihoji, je ni kweli tuna nia ya dhati ya kuleta maendeleo, kisha tunapopata majibu tuwe tayari kuyakubali na kubadilika. Kwanza tuwe na vision (maono) iliyo wazi itakayopitishwa na kukubaliwa na inayojenga shauku kwa wadau wote wakubwa kwa wadogo wa biashara nchini ambayo kila mmoja kwa hiari atakuwa tayari kulipa gharama ya maumivu kwa ajili ya maendeleo tunayotaka, pili faida ya mzalisha ndiyo iwe kiini cha msukumo wa utungaji sera, sababu yeye akifaidika sana na Serikali itafaidika sana kwa kodi, tatu kuwe na chombo kimoja cha udhibiti wa mapato.**

**Adam Ihucha**, Mwananchi

Takriban mwaka mmoja uliopita, Bunge lilipitisha sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) huku kuikiwa na matumaini kwamba itaboresha ukusanyaji wa mapato.

Lakini kama wahenga wasemavyo; "si kila king'aacho ni dhahabu," sheria hiyo nayo imegeuka kuwa adui mkubwa katika kilimo cha mbogamboga na maua.

Sheria hii mpya, utekelezaji wake ulianza Januari 2015, haitoi msamaha wa kodi kwa baadhi ya pembejeo muhimu za kisasa za kilimo kama vile vifaa vya umwagiliaji pamoja na vipuri vyao.

Vifaa vya kulinda mazao ambavyo siyo tu vinatumika katika kilimo cha mbogamboga, bali pia cha mazao ya biashara kama vile kahawa na pamba, navyo pia havijasamehewa. Vifaa vingine ambavyo havijapatiwa msamaha ni vile vya kuhifadhi na kupoza (kutunza) mbogamboga na maua.

Uongozi wa Chama cha Wakulima wa Mbogamboga na Maua (Taha) unasema, kilimo hicho hupoteza kati ya asilimia 30 na 60 ya mapato yanayostahili kwa mwaka kutokana na kukosa pembejeo madhubuti na vifaa vya kuvunia na kuhifadhi.

"Kuacha kuviondolea kodi vifaa vyote hivi, kuna maana kwamba, tutaendelea kupata hasara baada ya kuvuna na pengine kupunguza mapato ya nchi yatokanayo na sekta hii," anasema meneja wa utetezi wa Taha, Anthony Chamanga.

Ujenzi wa eneo moja la kuhifadhia mazao ya mbogamboga na maua, maarufu kwa jina la jingo, unasemekana kugharimu karibu Sh3 bilioni na kwamba kuongeza kodi juu ya gharama hizi kunakatisha tamaa uwekezaji mpya.

"Jengo moja la kuhifadhia linaweza kutunza mazao ya thamani ya Sh120 bilioni," anasema Chamanga.

Kilimo cha mbogamboga kinakadiriwa kuiliingizia Taifa Dola 500 za Marekani kwa sasa kutokana na mauzo ya mazao ya nje. Kiwango cha fedha kimeongezeka ikilinganishwa na Dola 64 zilizopatikana mwaka 2004.

"Fedha za kigeni, ajira kwa Watanzania pamoja na kodi zingine ni vitu ambavyo tungeweza kunufaika navyo iwapo ingeondolewa kodi ya ongezeko la thamani ambayo inafikia Sh540 bilioni kwa jengo moja," anaeleza Chamanga.Hata nyavu za kilimo, ambazo hutumika kuzuia wadudu na kuwaepushia wakulima gharama ya kununua dawa ghali za kuua wadudu, nazo hazijaondolewa kodi. Nyavu za kilimo ni maalumu kwa ajili ya kufunika mazao ya mbogamboga na hivyo kuyalinda kutokana na wadudu na maradhi mengine.

Nyavu hizo siyo tu huwapunguzia wakulima gharama za kuzalishia bali pia huwafanya waepukane na matumizi ya kemikali katika uzalishaji wao na hivyo kuwawezesha wazalisha mboga salama kabisa.

Wakulima wa mbogamboga wanasema, kuendelea kutoza VAT katika baadhi ya vifaa vya kilimo kunadumaza ukuaji wa sekta hiyo na kukatisha tama wawekezaji wapya, huku uwezekano wa kuongezeka mfumuko wa bei ukiwa mkubwa zaidi ikizingatiwa kwamba bidhaa za chakula huchangia asilimia 55.9 katika bidhaa zinazotumika kukokotoa mfumuko wa bei.

Jeremiah Thomas ambaye ni mkulima wa mbogamboga katika eneo la Nduruma, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha anasema, hata juhudi zinazofanywa na wadau wa maendeleo kusaidia maendeleo ya kilimo hicho kwa kuleta teknolojia mpya huenda zisizae matunda kutokana na kodi hiyo.

"Teknolojia mpya inakuja lakini sheria hii mpya ya VAT inaifanya kuwa ghali na hapo wakulima hawamudu bei," anaeleza Thomas. Shirika la Misaada la Marekani (USAID) limewekeza Dola 25 milioni za Marekani ndani ya miaka mitano iliyopita ili kuwasaidia wakulima wadogo wa mbogamboga kwa kuimarisha miundombinu pamoja na teknolojia. Ofisa mtendaji mkuu wa Taha, Jacqueline Mkindi anasema, sheria hiyo mpya ya VAT siyo tu inaongeza gharama za uzalishaji bali pia inakwamisha juhudi za kuendeleza kilimo na biashara nchini, suala ambalo ni ajenda kubwa kabisa. Anaeleza kwamba hali hiyo ni kuongeza mzigo kwa mkulima, huku akikabiliwa na kodi na tozo zingine zipatazo 45.

"Naishukuru Serikali kwani imeonyesha mwelekeo katika kushughulikia suala jambo hilo. Taha pamoja na Taasisi ya BEST-Dialogue, inayopigania uboreshaji wa mazingira ya kibiashara, tunalifanyia kazi hili," anasema. Mshauri mwelekezi wa masuala ya uchumi Balozi Marwa anasema, gharama ya kutoza VAT katika pembejeo za kilimo ni zaidi ya kuibagua sekta ya kilimo.

Anasema hali hiyo inaweza kuongeza bei za vyakula pamoja na kuathiri vitu vingine kama biashara kutokana na muunganiko wa kilimo na sekta nyingine.

"Kuongezeka kwa bei, huku hakutamsaidia Mtanzania wa kawaida na wala hakutamwongezea kipato mkulima kwani fedha inayoongezeka ni kodi ya Serikali," anaeleza.

Baadhi ya wachambuzi wa mambo wanasema ukuaji wa kilimo cha mbogamboga na maua unahitaji kusaidiwa kwani huenda ukaziba mapengo na kuchukua nafasi ya mazao ya asili kama kahawa na pamba ambayo hayafanyi vizuri kwa sasa.

"Wakulima wengi wa kahawa sasa wanahamia katika kilimo cha mbogamboga ambacho ni rahisi. Mustakabali wa kahawa nao siyo mzuri maana zao hilo huchukua muda mrefu na wakati huo bei yake ikidhibitiwa na soko la dunia," anasema Dk Gasper Mpehongwa, mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Tumaini.

***Kwa maoni kuhusu mazingira ya kibiashara Tanzania tuma ujumbe kwenda 0786240172. Ujumbe utakaochapishwa utazawadiwa Sh30,000 za muda wa maongezi.***

**NUKUU**

**VAT siyo tu inaongeza gharama za uzalishaji bali pia inakwamisha juhudi za kuendeleza kilimo na biashara nchini.**

Jacqueline Mkindi

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo